# JARIDA LA WAKILI MKUU

ISSN 2686 - 2686 | Toleo la Kumi na Tatu | Oktoba, 2024 - Aprili, 2025

## Miaka 4 ya Mafanikio ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali



## DKT. ALLY POSSI
WAKILI MKUU WA SERIKALI

# BODI YA UHARIRI

## Mwenyekiti

**Alice Edward Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**Dennis Julius Buyekwa**
Afisa Habari

## Msanifu wa Jarida

**Nyamhoni Robert Chacha**
Afisa TEHAMA

## Wajumbe

**Saddy Rashid Sevingi**
Mkurugenzi Msaidizi Usuluhishi wa Nje

**Hangi Matekeleza Chang'a**
Mkurugenzi Msaidizi Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi

**Kiuye Mbwana Shemakame**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti

**ACPA Devota Mathew Ngulugulu**
Mhasibu Mkuu

**Mercy Rowland Kyamba**
Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

**Zuhura Mohamed Kussaga**
Mchumi Mwandamizi

# TAHARIRI



**Prisca Jackson Ulomi**
Mhariri Mkuu

Jarida la Wakili Mkuu Toleo la 13 likiwa ni jukwaa mhimu ambalo limeendelea kuwa kiungo cha uhabarishaji wa umma kati ya ofisi ya Wakili Mkuu wadau wake katika kufikisha ujumbe mahususi ndani na nje ya nchi.

Awamu hii Toleo la 13 la Jarida la Wakili Mkuu litaendelea kutangaza majukumu yote yaliyotekelezwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kipindi cha kuanzia mwezi oktoba mpaka mwezi Aprili 2025 ili kuweza kuwafahamisha masuala yote muhimu ambayo yametekelezwa katika kipindi hicho ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia serikali kupiga hatua katika kuwaletea wananchi wake maendeleo ya kiuchumi, kisisa na kijamii.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kuhakikisha inatangaza yale masuala yote muhimu ambayo yametekelezwa na kuleta manufaa muhimu kwa taifa ikiwa ni pamoja na kuendesha mashauri kwa weledi mkubwa na kupelekea kuokoa fedha nyingi ambazo zingelipwa kwa wadai endapo serikali ingeshindwa mahakamani badala yake fedha zilizookolewa zimeelekezwa kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo ambayo itasaidia wananchi kupiga hatua katika Nyanja mbalimbali za maendeleo.

Ziara alizofanya Wakili Mkuu wa Serikali kwa sehemu kubwa zimeendelea kuimarisha ushirikiano kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na taasisi hizo hasa benki ya dunia ambapo viongozi hao walitumia fursa hiyo kujadili maeneo mbalimbali wanayoweza kushirikiana katika kuwajengea uwezo mawakili wa serikali kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa kuangalia programu mbalimbali za kisheria na sisizo za kisheria kwa watumishi ambao sio wanansheria ili kuimarisha utendaji wao katika kushughulikia mashauri ya serikali kwa ufanisi zaidi.

Aidha, Dkt. Possi ameiomba Benki ya Dunia kuangalia uwezekano wa kusaidia fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, hususani katika kusaidia ujenzi wa majengo ya Ofisi katika kila mkoa ambao una Mahakama Kuu ya Tanzania ili kupanua wigo wa uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi nchini.

Maadhimisho ya Wiki Sheria nchini yameendelea kuwa na umuhimu mkubwa katika kuendelea kutoa msaada wa kisheria nchini kwa wadau wa ofisi hii kwa kuendelea kutatua migogoro mbalimbali ikiwemo ya

ardhi na mirathi kwa njia ya majadiliano na hivyo kuleta Amani, utulivu na upendo katika jamii. Kama mdau muhimu Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendelea kutumia maadhimisho ya Wiki ya Sheria kama jukwaa muhimu ambapo pamoja na masuala tajwa hapo juu iliendelea kutangaza utekelezaji wa majuku yake kupitia maadhimisho hayo.

Katika kipindi husika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imeendelea kuwashirikisha mipango mbalimbali ikiwemo masuala ya kibajeti, na namna ya kutatua changamoto mbalimbali kwa watumishi wake wa makao makuu na ofisi za mikoa kwa kutumia mikutano na vikao vya baraza la wafanyakazi ambavyo vimekuwa vikifanyika mara mbili kwa mwaka.

Uwepo wa mabara ya wafanyakazi mahala pa kazi yameendelea Kuboresha Mawasiliano na Uhusiano wa Kazi kwa kuwa mabaraza hayo yamesaidia kuweka utaratibu mzuri wa mawasiliano ya pamoja kati ya viongozi wa taasisi na wafanyakazi. Hii inasaidia kupunguza migogoro, kwani malalamiko mahala pa kazi yanaweza kujadiliwa mara moja na kupatiwa suluhu kwa wakati.

Kupitia Toleo la 13 la Jarida la Wakili Mkuu ni matumaini yangu kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kutetea na kulinda maslahi mapana ya Serikali kwa kuendelea kuweka mipango madhubuti na endelevu katika kuhakikisha inaendelea kuokoa fedha nyingi ili kutimiza azima ya Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo na Taifa kwa ujumla.

# Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri



**Alice Edward Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya na siha njema. Ni wakati mwingine tena ambao natumia jukwaa hili adhimu kuleta kwenu ujumbe mahususi kutoka kwenye dawati la mwenyekiti wa Jarida la Wakili Mkuu kwa wadau wote na wasomaji wa Jarida hili kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inayodhamana kubwa ya uendeshaji wa Mashauri ya Madai, Usuluhishi Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi katika kuhakikisha kuwa inatimiza azma ya Viongozi na Watumishi wa Ofisi hii ambayo ni kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuwa ofisi muhimu katika taifa hili kwa kuwa imeendelea kusimamia kwa weledi na ufanisi mashauri yote yanayofunguliwa na serikali au dhidi yake katika kuhakikisha Serikali inapata haki zake zote hatua ambayo kwa kiasi kikubwa imepelekea ofisi hii kuendelea kuwa kiungo muhimu katika kuuunga mkono juhusu za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuwaletea wananchi wake maendeleo katika sekta zote ikiwemo ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo ni barabara za rami nchi nzima, madaraja makubwa ya kigongo busisi na wami, reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na Mwanza, miradi ya ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere na Kidunda na ujenzi wa vituo vya afya nchi nzima.

Aidha, kupitia toleo la 13 la Jarida la Wakili Mkuu, naomba kutumia jukwaa kwa wasomaji wote ndani na nje ya nchi kueleza mafanikio mbalimbali yaliyopatikana ndani ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) pamoja na mwelekeo wa ofisi hiyo katika kusaidia jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, katika kuwaletea wananchi maendeleo kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050.

Katika kipindi cha Jarida husika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imetekeleza majukumu yake kwa mafanikio makubwa ambayo ni pamoja na kuendelea kuimaimarisha mifumo ya kidijitali kwa ajili ya ufuatiliaji wa migogoro na uimarishaji wa haki, mifumo hii inalenga kuwezesha Serikali kupata takwimu sahihi kuhusu migogoro inayoshughulikiwa, muda wa utatuzi na kiwango cha mafanikio ya

migogoro inayosimamiwa, hatua inayosaidia kujenga jamii imara isiyo na migogoro na kuhakikisha wananchi wanaishi kwa amani ili waweze kuendelea na shughuli zao za kujiletea maendeleo.

Jarida hili pia limeangazia namna OWMS ilivyoendelea kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi kwa weledi ili kuhakikisha rasilimali za nchi zinalindwa, ikiwemo miradi mikubwa ya maendeleo kama vile Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere, Mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani (Tanga), na ujenzi wa madaraja makubwa ya Tanzanite na Kigongo-Busisi. Miradi hii imekuwa chachu ya maendeleo katika kujenga na kukuza uchumi wa nchi.

Kama tunavyofahamu kuwa mwaka huu nchi yetu inaenda kushiriki Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani hivyo naomba kutoa wito kwa wananchi wote kote nchini kushiriki zoezi hili adhimu katika kuhakikisha wanachagua viongozi makini watakao waletea maendeleo.

Pia, naomba niendelee kutoa wito kwa Mawakili wa Serikali kote nchini kuendelea kuratibu, kusimamia na kuendesha kwa weledi mashauri yote ya uchaguzi na haki za binadamu yatakayofunguliwa baada ya uchaguzi kwa kuwa ni jukumu letu sote kama watetezi wa haki kuhakikisha kuwa tunalinda na kusimamia misingi ya sheria ili kuendeleza na kudumisha amani, utulivu upendo na mshikamano ambayo ni tunu ya Taifa ambayo itaendelea kuifanya nchi yetu kuendelea  kuwa kisiwa cha amani Afrika Mashariki na Kati na dunia nzima kwa ujumla.

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| UK. O9 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yaokoa Zaidi ya Shilingi Bilioni 602.5 |
| UK. 12 | Ziara ya Dkt. Ally Possi katika Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu ya Afrika |
| UK. 14 | Ziara ya Dkt. Ally Possi katika Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki |
| UK. 16 | Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria Yawasilishwa Bungeni |
| UK. 18 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yaendesha Shauri Kuhusu Vijiji vya Ololosokwan |
| UK. 20 | Wakili Mkuu wa Serikali Ahimiza Matumizi ya Mifumo ya Kidijitali Ufuatiliaji wa Migogoro, Uimarishaji wa Haki |
| UK. 23 | Wakili Mkuu wa Serikali Afanya Ziara kwa Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia |
| UK. 25 | Wakili Mkuu wa Serikali Afungua Mafunzo ya Uendeshaji wa Mashauri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Kwa Mawakili wa Serikali |
| UK. 29 | Wakili Mkuu wa wa Serikali Akutana na Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB |
| UK. 31 | Wakili Mkuu wa Serikali Azungumza na Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali |
| UK. 33 | Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Afungua Mafunzo ya Uadilifu |
| UK. 35 | Msajili wa Baraza la Masoko ya Mitaji Amtembelea Wakili Mkuu wa Serikali |
| UK. 36 | Wakili Mkuu wa Serikali Ashiriki Kuwapokea Mawakili Wapya 524 |
| UK. 40 | Tumieni Mfumo wa e-Mrejesho Kuboresha Mahusiano na Wadau |
| UK. 44 | Watumishi wa Umma ni Taswira ya Serikali |
| UK. 48 | Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali washiriki Siku ya Wanawake Duniani kwa Namna ya Kipekee |
| UK. 56 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yamuaga Mstaafu Wake wa Kwanza |

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania





**Dkt. Ally Possi**
Wakili Mkuu wa Serikali

## *Miaka 4 ya Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali*



**Alice Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yaokoa Zaidi ya Shilingi Bilioni 602.5

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) ilianzishwa tarehe 13 Februari, 2018 baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusaini sheria ya kuanzishwa kwake. Lengo kuu la kuanzishwa kwa OWMS ni kuratibu, kusimamia, kuendesha na kuiwakilisha Serikali katika mashauri yote ya madai, usuluhishi, katiba, haki za binadamu na uchaguzi yanayofunguliwa na Serikali au yaliyofunguliwa dhidi ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

Tangu kuanzishwa kwake Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa ikitekeleza majukumu yake ya kuratibu, kusimamia, na kuendesha mashauri yote ya Madai na Usuluhishi yanayofunguliwa dhidi au kwa niaba ya Serikali na Taasisi zake ndani na nje ya Nchi.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kufuata na kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Taratibu, na Miongozo mbalimbali inayosimamia shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuendelea kuimarisha ustawi wa sheria na haki nchini katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeshuhudia mafanikio mengi ambayo yamepatikana baada ya Ofisi hii kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha.

Hatua hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa kuokoa fedha nyingi ambazo zingelipwa kwa wadai kama Serikali ingeshindwa katika mahakama mbalimbali ndani na nje ya nchi. Hivyo, fedha hizo sasa zitaelekezwa kwenye miradi mikubwa ya maendeleo ikiwa ni kuunga mkono juhudi kubwa zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika kipindi husika ni pamoja na; Kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake kwa ufanisi katika mashauri ya Madai na Usuluhishi ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hili, Ofisi imeweza kuokoa fedha ambazo Serikali ingetakiwa kulipa iwapo ingeshindwa mashauri hayo. Ofisi pia imeongoza na kushiriki katika Timu za Serikali za Majadiliano na kufanikisha kumaliza mashauri/migogoro nje ya Mahakama.

Aidha, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilifanikiwa kuhitimisha mashauri ya madai yasiyohusisha fedha yakiwemo mashauri ya katiba, haki za binadamu, uwekezaji na biashara yakiwemo; Mashauri ya Alphonse Lusako dhidi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Skymax Elevators Limited dhidi ya Mwanasheria Mkuu na Wenzake; na Jeremiah Mtobesya na mwenzake

dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.Katika mwaka wa fedha 2023/24, Ofisi ilifanikiwa kusajili na kuendesha jumla ya mashauri ya madai 9,650. Kati ya mashauri hayo, mashauri 9,519 ni ya kitaifa (zaidi ya asilimia 60 ni mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi) na mashauri 131 ni ya kimataifa. Katika kuendesha mashauri hayo, mashauri 1,412 yalimalizika. kwa kumalizika mashauri hayo, Ofisi imeokoa jumla ya shilingi za kitanzania Bilioni Mia Tano Thelathini na Sita na Nukta Tano (536.5).

Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/24, Ofisi ilifanikiwa kushughulikia jumla ya mashauri ya usuluhishi 201. Kati ya mashauri hayo,170 ni ya usuluhishi wa ndani na 31 ni ya usuluhishi wa kimataifa. Kati ya mashauri 201 yaliyoshughulikiwa, mashauri 43 yalimalizika kwa njia ya majadiliano mahakamani na kwenye Mabaraza ya Usuluhishi. Ikumbukwe kuwa, kumalizika kwa mashauri haya, Ofisi ilifanikiwa kuokoa jumla ya shilingi Bilioni Sitini na Sita nukta Sifuri Mbili (66.02), Dola za Marekani Milioni Mia Nane Nukta Mbili (817.6) na EURO Milioni Mbili (2,000,000).

Katika Mwaka wa Fedha 2024/25 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea na mikakati mbalimbali ya kuboresha utendaji kazi wake. Hatua hizo zinajumuisha masuala yafuatayo; Kuweka mipango mikakati kwa ajili ya utoaji wa mafunzo ya ubobezi kwa mawakili kwenye masuala mbalimbali ikiwemo masuala ya mafuta na gesi, masuala ya mikataba ya ujenzi na masuala ya usuluhishi wa kimataifa. Ofisi inatarajia kutoa mafunzo hayo mapema mwezi Novemba, 2024 na mafunzo hayo yatakuwa ni endelevu.

Vile vile Ofisi itaendelea kuboresha maslahi ya watumishi kupitia maboresho ya miundo pamoja na mikakati mbalimbali inayoendelea kuwekwa na Ofisi; ikiwemo kuweka mifumo rafiki ya usimamizi wa mashauri ili kurahisha utoaji wa taarifa za Ofisi na kuboresha utendaji kazi.



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyesimama katikati) akiwa na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya maadhimisho ya Siku ya Sheria yaliyofanyika Jijini Dodoma.*

# Takwimu za Mashauri Yaliyoendeshwa Katika Mwaka wa Fedha 2023/24

| Mashauri ya Madai | Mashauri ya Madai | Kiasi Kilichookolewa |
| --- | --- | --- |
| Yaliyoendeshwa | Yaliyomalizika | Shilingi |
| 9,650 | 1,412 | Bilioni 536.5 |

| Mashauri ya Usuluhishi | Mashauri ya Usuluhishi | Kiasi cha fedha Kilichookolewa |
| --- | --- | --- |
| Yaliyoendeshwa | Yaliyomalizika | Shilingi Bilioni 66.02<br>Dola za Marekani Milioni 817.6<br>EURO Milioni 2 |
| 201 | 170 | |

# Ziara ya Dkt. Ally Possi katika Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu ya Afrika



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akimkabidhi Jarida la Wakili Mkuu Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mhe. Jaji Imani Aboud alipotembelea Mahakama hiyo kwa lengo la kujitambulisha na kuona namna Mahakama hiyo inavyotekeleza majukumu yake Jijini Arusha.*



*Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mhe. Jaji Imani Aboud akizungumza na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi na ujumbe wake (hayupo pichani) wakati wa ziara yake ya kujitambulisha na kuona namna Mahakama hiyo inavyofanya kazi Jijini Arusha.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ya, Mhe. Jaji Imani Aboud (hayupo pichani) alipofika Mahakamani hapo kujitambulisha na kuona namna inavyofanya kazi Jijini Arusha.*



*Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Ally Possi (wa nne kushoto) na ujumbe wake akiwa kwenye picha ya pamoja na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Mhe. Iman Daud Aboud mara baada ya kutembelea Mahakama hiyo iliyopo Jijini Arusha kwa lengo la kujitambulisha na kujionea namna Mahakama hiyo inavyotekeleza majukumu yake.*

# Ziara ya Dkt. Ally Possi katika Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki

*Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Ally Possi (kushoto) akimkabidhi zawadi ya Jarida la Ofisi ya Wakili Mkuu Rais wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki, Mhe. Jaji Nestory Kayobera mara baada ya kumalizika kwa mazungumzo baina yao yaliyofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Mahakama hiyo iliyopo Jijini Arusha.*






*Rais wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki Mhe. Jaji Nestory Kayobera akizungumza na Wakili Mkuu wa Serikali na ujumbe wake alipotembelea Mahakama hiyo kwa lengo la kujionea jinsi Mahakama hiyo inavyotekeleza majukumu yake.*

*Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Ally Possi akizungumza na Viongozi wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki iliyopo Jijini Arusha alipotembelea Mahakama hiyo kwa lengo la kujitambulisha na kujionea jinsi Mahakama hiyo inavyotekeleza majukumu yake.*



*Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Ally Possi (wa kwanza kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na Viongozi wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki, Rais wa Mahakama hiyo Mhe. Jaji Nestory Kayobera (aliyesimama katikati) Jaji Kiongozi Mhe. Yohane Masara mara baada ya mazungumzo yaliyofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Mahakama hiyo iliyopo Jijini Arusha.*





*Jaji kiongozi wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki Mhe. Yohane Masara akizungumza na Viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (ambao hawapo pichani) wakati wa ziara ya Wakili Mkuu wa Serikali alipotembelea Mahakama hiyo Jijini Arusha.*



*Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Ally Possi akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki mara baada ya kutembelea Mahakama hiyo iliyopo Jijini Arusha.*

# Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria Yawasilishwa Bungeni



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akitambulishwa Bungeni wakati wa kusoma Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.*



*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), akiwasilisha Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 Bungeni jijini Dodoma.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (katikati) akifuatilia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria iliyosomwa Bungeni na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt.Damas Ndumbaro (Mb).*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yaendesha Shauri Kuhusu Vijiji vya Ololosokwan



*Mkurugenzi Msaidizi Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Hangi Chang'a akizungumza mbele ya jopo la majaji (hawapo pichani) wanaoendesha shauri kwa ajili ya kupanga mwenendo wa uendeshaji wa rufaa ya shauri lililofunguliwa na Halmashauri ya Kijiji cha Ololosokwan na wenzake watatu kwenye Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyopo Jijini Arusha.*

*Rais wa Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mhe. Jaji Nestory Kayobera akiendesha shauri kwa ajili ya kupanga mwenendo wa uendeshaji wa rufaa ya shauri lililofunguliwa na Halmashauri ya Kijiji cha Ololosokwan na wenzake watatu kwenye Mahakama hiyo iliyopo Jijini Arusha.*




*Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa na Mawakili wa kujitegemea baada ya kupanga mwenendo wa uendeshaji wa rufaa ya shauri lililofunguliwa na Halmashauri ya Kijiji cha Ololosokwan na wenzake watatu kwenye Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki iliyopo Jijini Arusha.*




*Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakijiandaa kwenda mahakamani kusikiliza shauri kwa ajili ya kupanga mwenendo wa uendeshaji wa rufaa ya shauri lililofunguliwa na Halmashauri ya Kijiji cha Ololosokwan na wenzake watatu kwenye Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyopo Jijini Arusha.*



# Wakili Mkuu wa Serikali Ahimiza Matumizi ya Mifumo ya Kidijitali Ufuatiliaji wa Migogoro, Uimarishaji wa Haki

*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (wa kwanza kushoto) akizungumza na Mkurugenzi Msaidizi Kurugenzi ya Usimamizi wa Mashauri wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Bi. Hawa Mguruta alipotembelea Banda la Mahakama ya Tanzania kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika Jijini Dodoma.*



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi ametoa wito kwa taasisi zote za kisheria na wadau wa haki nchini kutumia mifumo ya kidijitali kupata takwimu sahihi zitakazowawezesha kufuatilia migogoro yote waliyoisikiliza ili kuhakikisha inamalizika kwa wakati.

Dkt. Possi ametoa wito huo tarehe 01 Februari, 2025 alipotembelea mabanda ya maonesho ya taasisi mbali mbali nchini zilizoshiriki Maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini yaliyofanyika kwenye viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

Dkt. Possi ameeleza kuwa matumizi ya mifumo ya kisasa yatasaidia kuboresha usimamizi wa haki na kuongeza uwajibikaji katika utatuzi wa migogoro ya kisheria. Hatua itakayowezesha kutoa takwimu sahihi na kwa haraka pale taasisi husika itakapohitaji kufahamu mwenendo wa migogoro husika iliyoshughulikiwa.

Akizungumza na watumishi wa Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt. Possi amesisitiza kuwa mifumo ya kidijitali ina uwezo mkubwa wa kuboresha utendaji kazi wa taasisi za kisheria kwa kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa wakati. Hatua itakayosaidia kuhakikisha migogoro yote inayoshughulikiwa kwenye kliniki za sheria inamalizika ili wananchi waweze kufanya shughuli zao za kukuza uchumi kwa amani.



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akiwa na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye banda la Ofisi hiyo alipotembelea Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika Jijijni Dodoma.*

"*Kwa kutumia mifumo ya kisasa, tunaweza kufuatilia mwenendo wa migogoro yote kwa urahisi ili kuhakikisha migogoro yote inasimamiwa kwa weledi na kupunguza ucheleweshaji wa haki ili wananchi waendelee na shughuli za kujiletea maendeleo yao na Taifa kwa ujumla*," alisema Dkt. Possi.

Alibainisha kuwa, matumizi sahihi ya mifumo hiyo yatasaidia kuondoa changamoto zinazoikabili Sekta ya Sheria nchini katika kushughulikia migogoro ikiwa ni pamoja na kupotea kwa nyaraka muhimu ambazo zimechangia ucheleweshaji wa maamuzi huku akisisitiza taasisi zinazohusika na usimamizi wa sheria kushirikiana katika kuunda na kutekeleza mifumo ya kidijitali inayolenga kuboresha uwajibikaji na uwazi.

Dkt. Possi alieleza kuwa mifumo hii itaiwezesha Serikali kupata takwimu sahihi kuhusu migogoro inayoshughulikiwa, muda wa utatuzi wa migogoro husika na kiwango cha mafanikio ya migogoro inayosimamiwa na kumalizika kwa mafanikio makubwa. Hatua hii itatimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha tunajenga jamii imara isiyo na migogoro kwa kuhakikisha wananchi wanaishi kwa amani ili waweze kuendelea na shughuli zao za kujiletea maendeleo.

Akizungumzia namna Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inavyochangia kukuza pato la taifa, Dkt. Possi amesema kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imehakikisha wakati wote kuwa rasilimali za nchi zinalindwa, ikiwemo miradi mikubwa ya maendeleo kama vile bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere, mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga, ujenzi wa madaraja makubwa ya Tanzanite na John Pombe Magufuli linalojengwa Jijini Mwanza. Miradi hii imekuwa chachu ya maendeleo katika kujenga na kukuza uchumi wa nchi.

“*Miradi inalindwa kwa kuhakikisha kuwa utekelezaji wake hauathiriwi wala kukwama kutokana na migogoro na pale inapotokea changamoto Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inasimamia ili kuhakikisha kuwa miradi haisimami, haikwami au kushindwa kutekelezwa kutokana na migogoro. Ofisi yetu imekuwa inashughulika kwa njia moja au nyingine katika uendelezaji wa miradi na kuhakikisha kuwa migogoro haiwi chanzo cha kuzuia utekelezaji wa miradi mbali mbali nchini*”, alisisitiza Dkt. Possi.

Ameongeza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuzishauri taasisi za Serikali ipasavyo pamoja na kumaliza mashauri nje ya Mahakama hatua ambayo imesaidia kupunguza migogoro na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Naye Afisa Mchunguzi Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria ndugu Laurent Bulilo amesema kuwa wamekuwa na kawaida ya kufuatilia migogoro na mashauri yote kupitia Mfumo wa Mama “Samia Legal Aid Campaign System” hatua ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza migogoro kwenye jamii.

Dkt. Possi ameonyesha jinsi Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inavyochangia kukuza pato la taifa kupitia usimamizi wa mali za umma, mikataba ya kimataifa na uimarishaji wa mazingira ya biashara.

Pia, ameahidi kuendelea kushirikiana na wadau wote wa sheria hasa wadau wa haki madai katika matumizi ya TEHAMA ili kuhakikisha mifumo inasomana ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali.




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akimsikiliza Afisa Uchunguzi Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, ndugu Laurent Bulilo alipotembelea banda la Wizara hiyo wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika Jijini Dodoma.*




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyesimama kushoto) akisalimiana na Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia anayesimamia nchi za Tanzania, Malawi, Zambia na Zimbabwe, ndugu Nathan Belete katika kikao kilichofanyika ofisini kwa Mkurugenzi huyo Jijini Dar es Salaam.*

# Wakili Mkuu wa Serikali Afanya Ziara kwa Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia

## Wajadili Ushirikiano Baina ya Ofisi Hizi Mbili



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza na Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia anayesimamia nchi za Tanzania, Malawi, Zambia na Zimbabwe ndugu Nathan Belete (hayupo pichani), alipomtembelea ofisi kwake Jijini Dar es Salaam.*



*Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia anayesimamia nchi za Tanzania, Malawi, Zambia na Zimbabwe, Bw. Nathan Belete akizungumza mara baada ya kumpokea Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Ally Possi na ujumbe wake (hawapo pichani) ofisini kwake Jijini Dar es Salaam.*



*Baadhi ya Viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) wakati wa kikao na Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia anayesimamia nchi za Tanzania, Malawi, Zambia na Zimbabwe, ndugu Nathan Belete kilichofanyika Jijini Dar es Salaam.*

# Wakili Mkuu wa Serikali Afungua Mafunzo ya Uendeshaji wa Mashauri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Kwa Mawakili wa Serikali





*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akifungua mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kuhusu Sheria, Taratibu na Kanuni za uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa yaliyofanyika mkoani Morogoro.*

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi amefungua mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yenye lengo la kuwajengea uwezo Mawakili hao kuhusu namna bora ya kuendesha mashauri ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa yanayotarajiwa kufunguliwa baada ya kuhitimishwa kwa uchaguzi uliofanyika nchi nzima tarehe 27 Novemba, 2024.

Akizungumza wakati wa kufungua mafunzo hayo, Dkt. Possi amesema kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri yote ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa kwa niaba ya Serikali na taasisi zake kwenye Mabaraza na Mahakama ndani na nje ya nchi. Mafunzo haya yatafanyika kwa siku mbili na yatatolewa na wakufunzi wabobezi wa Sekta ya Sheria ili kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali kwenye maeneo mbalimbali yanayohusu kanuni na taratibu za uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

"Tumeona ni muhimu kuendesha mafunzo haya ili kuwakumbusha Mawakili wa Serikali kanuni na taratibu zote za uendeshaji wa mashauri yanayohusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa yatakayofunguliwa ili waweze kuyasimamia kwa weledi na kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati," alisema Dkt. Possi.

Alieleza kuwa ili kulinda haki za msingi za watanzania wote kwa mujibu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na kupitia kanuni ya 44 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya za mwaka 2024, kanuni ya 41 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo za mwaka 2024, kanuni ya 44 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji za mwaka 2024, na kanuni ya 43 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji za mwaka 2024 zimeweka wazi kuwa mgombea yoyote ambae hakuridhika na matokeo ya uchaguzi au uendeshaji wa uchaguzi kuwa na haki ya kufungua shauri katika Mahakama ya Wilaya ndani ya siku thelathini tangu siku ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi husika.

Dkt. Possi aliongeza kuwa iwapo mgombea yeyote atafungua shauri la uchaguzi, shauri hilo litafunguliwa dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri husika au afisa aliyeteuliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataunganishwa kwenye shauri hilo.

Dkt. Possi alieeleza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itakuwa na jukumu la kusimamia na kuendesha mashauri ya uchaguzi kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wowote ambapo mlalamikaji atafungua shauri la uchaguzi Mahakamani.

Mafunzo hayo yalijikita kwenye mada mbalimbali ikiwemo uelewa wa jumla wa sheria zinazosimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tanzania; Taratibu za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa; maadili kwenye uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi; taratibu za uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi; Utafiti kwenye uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi; na ushahidi wa kieletroniki kwenye uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi.

Dkt. Possi alisema kuwa Serikali iliona ni muhimu kuwajengea uwezo Mawakili hao kwa kutoa mafunzo hayo baada ya kupata maoni ya wadau wa Sekta ya Sheria nchini ikiwemo Mahakama ya Tanzania kuhusu maeneo yanayopaswa kuboreshwa katika kutekeleza majukumu ya OWMS ya kuiwakilisha Serikali Mahakamani na kwenye Mabaraza mbalimbali katika uendeshaji wa mashauri ikiwemo mashauri yanayohusu uchaguzi hususani uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwaka huu.

Aidha, Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alitoa rai kwa Mawakili hao kuwa wasikivu wakati wa mafunzo hayo kwa kuwa ni matarajio yake kuwa baada ya mafunzo hayo Mawakili hao watapata uelewa wa kina kuhusu Kanuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kanuni za uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa na uendeshaji wa mashauri kwa ujumla ili waweze kuendesha mashauri ya uchaguzi kwa ufanisi, weledi na ujuzi na kuboresha usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya Serikali kwa kuzingatia utafiti, misingi ya uandaaji wa nyaraka za Mahakama, uandaaji wa mashahidi, namna ya kutoa ushahidi wa kielektroniki na masuala mengine yanayohusu uendeshaji wa mashauri kwenye Mahakama.

Katika hatua nyingine Dkt. Possi aliwataka watumishi hao kufanyia kazi yote watakayoelezwa sambamba na kuzingatia Kanuni na Maadili ya Utumishi wa Umma wakati wote katika kusimamia na kuendesha mashauri ya uchaguzi huku wakiendelea kuzingatia matumizi ya TEHAMA katika kusimamia mashauri hayo.

**"**Hivi Karibuni, nilitembelea Mahakama Kuu Geita, kujionea Mahakama mtandao, wenzetu wapo katika hatua ya kuachana na matumizi ya Karatasi na kila kitu kinaendeshwa kwa TEHAMA, nafikiri ni wakati sasa na sisi tuanze kuelekea huko kwani dunia haitusubiri", amesema Dkt. Possi.

Akitoa salamu za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa niaba ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo; Mkurugenzi wa Idara ya Madai, ndugu Mark Mulwambo amesema kuwa mafunzo haya ni mwendelezo wa mipango ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Mawakili wa Serikali waliopewa hati idhini ya kuendesha mashauri ya Serikali kwa niaba ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Mafunzo hayo yanatolewa kwa Mawakili wa Serikali kutoka Wizara na taasisi mbali mbali za Serikali.



*Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Sarah Mwaipopo akichangia mada ya umuhimu wa kufanya utafiti katika uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa wakati wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kuhusu Sheria na Taratibu za Uendeshaji wa Mashauri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yaliyofanyika mkoani Morogoro.*



*Jaji Msataafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Robert Makaramba akitoa mada kuhusu Maadili katika uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa wakati wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kuhusu Sheria na Taratibu za Uendeshaji wa Mashauri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yaliyofanyika mkoani Morogoro.*





# Wakili Mkuu wa wa Serikali Akutana na Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB

*Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Bi. Ruth Zaipuna akizungumza na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) alipomtembelea kiongozi huyo kwa lengo la kujitambulisha Ofisini kwake jijini Dar es Salaam.*





*Viongozi waandamizi kutoka Benki ya NMB wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) wakati wa ziara ya Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Bi. Ruth Zaipuna walipomtembelea Wakili Mkuu wa Serikali ofisini kwake jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujitambulisha.*

# Wakili Mkuu wa Serikali Azungumza na Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza na wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) wakati wa kikao cha Menejimenti ya ofisi hiyo kilichofanyika Jijini Dodoma.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akipitia taarifa ya Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wakati wa kikao cha Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika Jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Asha Hayeshi akiwasilisha taarifa ya Idara hiyo wakati wa kikao cha Menejimenti ya Ofisi hiyo kilichofanyika Jijini Dodoma.*



*Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) wakati wa kikao cha Menejimenti ya ofisi hiyo kilichofanyika Jijini Dodoma.*

# Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Afungua Mafunzo ya Uadilifu



**Alice Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo amefungua mafunzo kwa Kamati ya Uadilifu na kwa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani kwa muda wa siku mbili kuanzia tarehe 20 hadi tarehe 23 Novemba, 2024. Mafunzo hayo yalitolewa na wataalam wa Ofisi ya Rais, Ikulu.

Bi. Mtulo alifungua mafunzo kwa Kamati ya Uadilifu ya OWMS na kwa wajumbe hao ili wafahamu majukumu yao na kujipanga kuyatekeleza kwa kuzingatia matakwa ya Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Nne (NASCAP- 2023/2030). Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeunda Kamati ya Uadilifu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 kama ilivyorejewa 2019 pamoja na Waraka uliotolewa na Serikali wa kuzitaka Ofisi za umma kuanzisha Kamati za Maadili. Aidha, OWMS ilimteua Bi. Vivian Method kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uadilifu wa Ofisi hiyo.

Bi. Mtulo aliongeza kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuwapatia uelewa wajumbe wa Kamati kuhusu malengo ya kamati, wajibu wa wajumbe wa Kamati, namna Kamati zinavyotekeleza majukumu yake pamoja na kuelewa mategemeo ya Serikali kwa Kamati.

*''Mafunzo haya tuyachukulie kwa uzito wake na kwa umakini kwa kuwa hayatusaidii tu kwenye Ofisi bali hata kwenye maisha yetu nje ya Ofisi ili kujenga jamii inayoishi na kuzingatia maadili,''* amesisitiza Bi. Mtulo.

Pia, alitoa rai kwa washiriki kutumia fursa hiyo adhimu kupata mafunzo hayo na kwenda kufanyia kazi ipasavyo yale yote waliyofundishwa ili kuleta tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa manufaa ya Taifa na wananchi kwa ujumla.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (aliyesimama katikati) akiwa na wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kufungua mafunzo kwa wajumbe wa kamati ya Uadilifu ya Ofisi hiyo kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne yaliyofanyika Kibaha Mkoani Pwani.*



*Baadhi ya wajumbe wa Menejimenti na Kamati ya Uadilifu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo kwa wajumbe hao kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne yaliyofanyika Kibaha Mkoani Pwani.*

# Msajili wa Baraza la Masoko ya Mitaji Amtembelea Wakili Mkuu wa Serikali



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyeketi kushoto) akimsikiliza Msajili wa Masoko ya Mitaji ndugu Martin Kolikoli kwenye kikao kilichofanyika Ofisini kwa Wakili Mkuu wa Serikali Jijini Dar es Salaam. Ndugu Kolikoli amemtembelea Wakili Mkuu wa Serikali kwa lengo la kujitambulisha na kumueleza namna ofisi yake inavyotekeleza majukumu yake.*



*Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Ally Possi (aliyesimama kushoto) akimkabidhi Jarida la Wakili Mkuu, Msajili wa Baraza la Masoko ya Mitaji Ndg. Martin Kolikoli alipomtembelea Wakili Mkuu wa Serikali kwa lengo la kujitambulisha ofisini kwake Jijini Dar es Salaam.*

# Wakili Mkuu wa Serikali Ashiriki Kuwapokea Mawakili Wapya 524



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi amewataka mawakili wapya 524 kufanya kazi kwa bidii huku wakizingatia misingi ya uendeshaji wa mashauri na taaluma ya sheria hatua itakayosaidia kukuza taaluma zao ili kuweza kufikia malengo yao.

Pia, aliwaasa kuepuka kujihusisha na vitengo visivyofaa kama vile rushwa ili kuendelea kuipa heshima taaluma ya sheria nchini kwa kuwa sheria ndio msingi wa kila kitu katika kulisaidia taifa kuendelea kupiga hatua katika kuwaleta wananchi wake maendeleo.

Hayo yalizungumzwa na Dkt. Possi aliposhiriki hafla ya kuwapokea na kuwakubali Mawakili wapya 524 iliyofanyika kwenye viwanja vya Karimjee Jijini Dar es Salaam.

Naye Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma, aliwataka Mawakili hao kuendelea kuzingatia nguzo tano za uweledi za uwakili wanapotekeleza majukumu yao, ikiwemo kuwa waaminifu na kujisimamia.

Akizungumza katika sherehe hizo zilizofanyika katika Viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam, Mhe. Prof. Juma ametaja nguzo nyingine kuwa ni uwezo, kupata heshima, kuwa na ujasiri na kufanya kazi kwa uhuru bila shinikizo kutoka upande wowote.



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akitambulishwa wakati wa sherehe ya kuapisha Mawakili wa Kujitegemea iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

Aliongeza kuwa Uweledi katika kazi ya Uwakili ni kanuni, tamaduni, tabia, mazoea na taratibu ambazo zimekubaliwa kuwa zinawaongoza Mawakili katika kazi na zinawatambulisha, kuwapambanua na kuwatofautisha na taaluma zingine.

Akizungumzia nguzo hizo, Jaji Mkuu amesisitiza kuwa lazima kila Wakili awe na uwezo wa kutambua kuwa uaminifu na kuaminika ni nyenzo itakayompambanua kuwa ni Mawakili mwenye uweledi au la.

Alieleza kuwa vipimo na vigezo vya uaminifu na kuaminika kwao vimetajwa katika Kanuni za Kimaadili, Kiweledi, Nidhamu na Tabia Njema za Mawakili. Kanuni ya 6 ya Kanuni hizi imeainisha mifano ya Mawakili wasio waminifu na kukosa uaminifu ni kukosa weledi hivyo ameitaka jamii ya watanzania kuepuka aina ya mawakili wa aina hiyo.

Kuhusu nguzo ya uwezo, Mhe. Prof. Juma alibainisha kuwa kwa vitendo, kwa kauli na kwa viwango vya huduma, lazima Wakili aoneshe kuwa kweli amesoma Sheria na Shahada ya Sheria na kwamba maandishi na fikra zake zijionyeshe kuwa yeye ni mwanasheria na ni Wakili.


Alieleza kuwa Kanuni za Maadili, Weledi, Nidhamu

na Tabia Njema za Mawakili za Mwaka 2018 zinataka huduma za Wakili zionyeshe uwezo na ujuzi unaotarajiwa kutoka kwa Wakili na mwanasheria aliyesoma chuo kikuu na kuiva.

"Kanuni za 8 hadi 14 za Kanuni za Maadili, Weledi, Nidhamu na Tabia Njema za Mawakili, 2018 zinasisitiza wateja wenu, Mahakama na wananchi wanayo haki ya Mahakama.

"Kila Wakili, anao wajibu wa kujisimamia na kuwasimamia Mawakili wenzake ili watekeleze kanuni zinazosimamia Uweledi na Uadilifu wa Mawakili. Kudharau au kutokutekeleza Kanuni zenu wenyewe, ni kuhujumu Uhuru wa Taaluma ya Uwakili na pia manufaa ya umma ambayo Kanuni Wakili, anayeheshimika na kuwaheshimu Mawakili wenzake, anawaheshimu wateja wake, Majaji, Mahakimu na watumishi wote katika mfumo mzima wa utoaji wa haki," amesema.

Mhe. Prof. Juma alibainisha pia kuwa Wakili mwenye Weledi au Ubobezi ni kama jengo imara lisilo na nyufa na wananchi watakaofuata huduma za




*Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Juma akizungumza na Mawakili wapya wakati wa tukio la kuwapokea na kuwakubali Mawakili hao kwenye hafla iliyofanyika kwenye viwanja vya Karimjee, Jijini Dar es Salaam.*

kutarajia kuwa mnao uwezo kufanya kazi ya uwakili itakayokuwa inawakabili," Jaji Mkuu amesema.

Mhe. Prof. Juma alibainisha pia kuwa kupitia Chama cha Mawakili, Mawakili wanatakiwa kujisimamia, kujiendesha kiuweledi, kimaadili na kitaaluma bila kuingiliwa na Taasisi za Dola kama Serikali, Bunge na zenu za Uweledi na Uadilifu zinalenga," amesema.

Jaji Mkuu amewaambia Mawakili hao pia kuwa katika safari yao ya kufikia uweledi, watatafuta nguzo muhimu ya kupewa "Heshima" bila ya kuiomba au kuidai.

"Heshima hapa ni kwa tabia na mwenendo wa Wakili, kila siku na kila wakati. Jamii inampa heshima Wakili, hawatakuwa na sababu za kuhofia madhara yoyote. Alisema kuwa sifa zake humtangaza Wakili aliyetimiza safari na kufikia nguzo zote za uweledi na uadilifu.

Akizungumza katika sherehe hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Johari amewaambia Mawakili hao kuwa wanayo nafasi kubwa



*Sehemu ya Mawakili wapya wakila kiapo.*

katika kuhakikisha jukumu la utoaji haki linatekelezwa kwa ufanisi na Mahakama.

Alisema kuwa kama Maafisa wa Mahakama Mawakili wanapaswa kuhakikisha wanaisaidia Mahakama kutekeleza jukumu la utoaji haki nchini kwa kutoa tafsiri sahihi za sheria ili kutenda haki na kuhakikisha wananchi wanapatiwa haki zao wanapokwenda mahakamani au kwenye vyombo vingine vya kisheria.


Katika harakati zenu za kusimamia haki, ni muhimu kujua kuwa jukumu lenu ni kubwa zaidi ya kuwawakilisha wateja. Ninyi ni walinzi wa haki, wawakilishi wa uadilifu, na watetezi wa sheria katika jamii yetu. Malalamiko ya wananchi kuhusu kutotendewa haki yatapungua kwa kiasi kikubwa mkitimiza wajibu wenu kikamilifu," Mhe. Johari amesema.

Naye Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), Wakili Msomi Boniface Mwambukusi amewaeleza Mawakili hao kujenga tabia ya kuheshimu maamuzi yanayotolewa na Mahakama katika ngazi mbalimbali.

"Ukiona haujaridhika, kata rufaa," amesema na kuwasisitizia Mawakili hao wapya kuwa lazima watambue kuwa kazi yao inatokea ndani ya mfumo wa Mahakama, ambayo ni nguzo muhimu katika utawala wa Sheria na utoaji wa haki.

"Kama wawakilishi wa sheria, mnajukumu la kuheshimu Mahakama kama taasisi. Mahakama siyo tu sehemu ya kutoa hukumu, bali pia ni chombo cha kuhifadhi na kutetea haki za kila mtu.

Kupokelewa kwa Mawakili hao wapya 524 kunafanya idadi ya Mawakili wa Kujitegemea nchini kufikia 12,995. Kati ya Mawakili hao wapya 524, wa kiume ni 296 na wa kike ni 228.



*Mawakili wapya wakitoa heshima kwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Juma (hayupo pichani).*




*Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Juma (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi mbalimbali baada ya kuwaapisha Mawakili wapya jijini Dar es Salaam.*

# Tumieni Mfumo wa e-Mrejesho Kuboresha Mahusiano na Wadau



*Mkurugenzi Msaidizi sehemu ya Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Hangi Chang'a akizungumza na baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti na watumishi wa Ofisi hiyo (ambao hwapo pichani) wakati akifungua Mafunzo kuhusu Matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Afisa Utumishi Mwandamizi wa Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bi. Mwadawa Nchemwa akitoa ufafanuzi kuhusu Mapitio ya Mfumo wa majukumu ya Wakuu wa Idara na Vitengo katika Mfumo wa e- Mrejesho wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*

***"Kupitia Mfumo wa e-Mrejesho ndipo taasisi zinaweza kuboresha huduma, kujirekebisha pale zinapokosea, kuweka mikakati mbalimbali na kuongeza ufanisi"***

Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, wametakiwa kutumia mfumo wa e-mrejesho kuboresha mahusiano na wadau ili kuhakikisha ufanisi na tija katika kutoa huduma kwa wadau.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Madai Sehemu ya Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi ndugu Hangi Chang'a wakati akifungua mafunzo kuhusu matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho kwa niaba ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Kibaha mkoani Pwani.

Akizungumza na Wajumbe wa Menejimenti na baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walioshiriki mafunzo hayo, Chang'a alisema kuwa kwa sasa Serikali inaboresha utoaji wa huduma kwa kuwekeza katika teknolojia ambapo tumeshuhudia mifumo mingi ya kielektroniki ikianzishwa ili kuongeza ufanisi na kutoa huduma bora.

Aliongeza kuwa Mfumo huu wa e-mrejesho ambao ulifundishwa ni mojawapo ya mikakati ya Serikali katika kuhakikisha huduma zinaboreshwa. Kupitia mfumo huu taasisi za umma na wananchi wanaweza kupata mrejesho wa huduma zinazotolewa kwa haraka na urahisi zaidi ukilinganisha na zamani ambapo iliwalazimu wananchi kusafiri umbali mrefu kufuata taarifa mbalimbali walizokuwa wanazihitaji kutoka kwenye taasisi husika.

Ndugu Chang'a alieleza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kama taasisi ya umma inaunga mkono juhudi za Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan. Serikali ya Awamu ya Sita imeweza kutumia mfumo huu, maelekezo ambayo yalitolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuwa kila taasisi ya Serikali lazima itumie mfumo huu ili kuhakikisha wanapata mrejesho wa huduma wanazotoa hatua itakayosaidia kuboresha huduma kwa wananchi.

Kiongozi huyo alieleza kuwa, taasisi za umma zinatoa huduma kwa wananchi na wadau mbalimbali na kupitia huduma hizo taasisi zinapaswa kupata mrejesho wa huduma zinazotolewa, ili ziweze kupata fursa ya huduma zake kwa wananchi wanaowahudumia.

***"kupitia mrejesho ndipo taasisi zinaweza kuboresha huduma, kujirekebisha pale zinapokosea, kuweka mikakati mbalimbali, kuongeza ufanisi". alisema Chang'a.***

Ndugu Chang'a amefafanua kuwa mafunzo haya yataisaidia OWMS kupata mrejesho kutoka kwa wadau na wananchi wanaohudumiwa na hivyo kujifanyia tathmini na kuboresha huduma zinazotolewa.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa kupitia mafunzo hayo washiriki watapata nafasi ya kufundishwa masuala mbalimbali kuhusu dhana nzima ya mrejesho, mwongozo wa ushughulikiaji mrejesho na huduma



*Baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Afisa Utumishi wa Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ndugu Hassan Kilenza (hayupo pichani) wakati akitoa mada kuhusu Mwongozo wa ushughulikiaji wa mrejesho na shughuli zinazotolewa na Serikali wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*

zinazotolewa na Serikali. Pia ,walifundishwa majukumu ya wakuu wa idara na vitengo katika mfumo wa e-mrejesho pamoja na wajibu wenu katika mfumo huu.

Kiongozi huyo alitumia mafunzo hayo kuwasihi watumishi kushiriki kikamilifu kwenye mafunzo ili yawe na tija kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Baada ya mafunzo haya watekeleze ipasavyo yote waliyofundishwa na kuongeza kuwa kama viongozi mnategemewa kuwa mfano kwa watumishi mnaowaongoza.

Naye Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Asha Hayeshi aliushukuru uongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kukubali kutoa mafunzo hayo kwa wajumbe wa Menejimenti na kuahidi kuwa atakwenda kuusimamia mfumo huo ipasavyo ili uweze kuleta tija katika kuhudumia wadau wa ndani na nje ya ofisi hiyo.

Aliongeza kuwa Mfumo wa e-mrejesho ni sehemu ya jitihada za Serikali kuboresha utendaji kazi na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Hivyo, ni vyema mfumo huo ukatumika ipasavyo ili kutusaidia kupata mrejesho kuhusu huduma tunazozitoa.

Bi. Hayeshi aliwahimiza viongozi wa Ofisi kujifunza mfumo wa e-mrejesho ili kuwaelekeza watumishi wanaowasimamia. Lengo likiwa ni kuboresha utendaji kazi ili kuongeza ufanisi serikalini.



*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Asha Hayeshi akitoa neno la utangulizi kwa baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya ofisi hiyo wakati wa Mafunzo kuhusu Matumizi ya Mfumo wa e- Mrejesho yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*

# Watumishi wa Umma ni Taswira ya Serikali

*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akizungumza wakati wa mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



**Alice Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

Watumishi wa umma ni taswira au sura ya Serikali hivyo tunatakiwa tuangalie na kuzingatia namna tunavyofanya kazi na tunapotekeleza majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa niaba ya Serikali. Kila mmoja ana wajibu wa kutunza taswira ya Serikali tunayoitumikia chini ya Uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hayo yalisemwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo wakati wa kufunga mafunzo elekezi kwa watumishi wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaliyofanyika kwa muda wa siku tano Kibaha mkoani Pwani.

Bi. Mtulo aliwaeleza watumishi hao kuwa Serikali ina sheria, taratibu na kanuni zinazowapa mwongozo wa namna ya kufanya kazi kama mtumishi wa umma, ambapo katika hayo maadili ya utumishi wa umma, yanatuasa kutojihusisha na rushwa.

"*Sisi ni Mawakili wa Serikali, tunaendesha mashauri yenye maslahi mapana ya Serikali ambapo mashauri hayo yana kiwango kikubwa cha fedha na yanahusisha watu mbalimbali ndani na nje ya nchi, hivyo Mawakili wa Serikali tujiepushe na rushwa. Aidha, inapotokea unakutana na mazingira ya rushwa, jiepushe ili kulinda taswira ya taasisi na Serikali; heshima; utu na haiba yako kwa jamii na watu wanaokutegemea,"* alisisitiza Bi. Mtulo.

Bi. Alice Mtulo amewataka Mawakili hao kutunza siri za Serikali kwa kuwa majukumu

wanayotekeleza yanawapa nafasi ya kufahamu taarifa nyeti. *"Jinsi unavyotunza siri zako, una wajibu wa kutunza siri za Serikali, tuwe waangalifu katika hili. Ukikutwa umevujisha taarifa za Serikali utachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria,"* alifafanua Bi. Mtulo.

Aidha, aliwaasa Mawakili hao kuzingatia mawasiliano na uhusiano baina yao na viongozi, watumishi wengine na wadau wanaofanya nao kazi. Alisisitiza kuwa na mipaka kwa kuzingatia taratibu za Ofisi ikiwemo kuwa makini kwa yale wanayoandika na kuongea ikiwa ni pamoja na kufuata sheria, kutumia hekima na busara, kuwa waaminifu na wasikivu kwa Serikali tunayoitumikia.

"Sipo tayari kumvumilia mtu yeyote asiyekuwa na nidhamu kwake yeye mwenyewe, wenzake na kwa kiongozi wake.

Vilevile, alitoa rai kwa Mawakili hao kuzingatia na kutumia mifumo ya TEHAMA kwa kuwa Serikali imejikita kwenye matumizi ya mifumo ya TEHAMA. Ofisi ina mifumo mbalimbali ya TEHAMA ambapo kila mtumishi atapimwa utendaji kazi wake kupitia mifumo hiyo. Alisisitiza kuwa kila mmoja anapaswa kujaza taarifa za utekelezaji wa majukumu kupitia mifumo hiyo. "*Ukitoka Mahakamani jaza taarifa kwenye mifumo husika ili Ofisi ipate takwimu sahihi na kwa wakati.*" Aidha alisisitiza kuhusiana na dhumuni na wajibu wa kila mmoja kwa Ofisi, wajibu kwa wafanyakazi wenzako na wajibu kwako wewe binafsi. "Kumbuka na tafakari kuwa ulikuja Ofisini peke yako, usifuate mikumbo na usiwe mwanaharakati. Zingatia sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma, endapo una mahitaji ya msingi wasilisha kwa mamlaka husika kwa utaratibu uliowekwa na yatafanyiwa kazi," amefafanua Bi. Mtulo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi hiyo, Bi. Asha Hayeshi amewaeleza Mawakili hao kuwa ni muhimu kwa Wakili wa Serikali kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na watumishi wenzake ili kurahisisha mgawanyo wa majukumu na matumizi bora ya ujuzi kwa kila mmoja wakati wa kuandaa majibu ya mashauri ya Serikali, kuchambua ushahidi kwa kina na kuhakikisha mashauri yanaendeshwa kwa ufanisi mkubwa kwa maslahi mapana ya Serikali.



*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Asha Hayeshi akiwasilisha mada kuhusu Muundo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya wa ofisi hiyo yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Prisca Ulomi akiwasilisha mada kuhusu Mawasiliano na Uhusiano kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa mafunzo elekezi kwa watumishi hao yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Baadhi ya Waajiriwa wapya wa ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Mhadhiri Mkuu wa Idara ya Kumbukumbu, Nyaraka na Taarifa wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Ndugu Said Hassan (hayupo pichani) wakati wa mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya wa ofisi hiyo yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Wakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Ditrick Luambano akichangia mada kuhusu Muundo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya wa ofisi hiyo yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Afisa Kumbukumbu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Athumani Zunda akitoa mada kuhusu Ofisi Mtandao (e-Office) kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa mafunzo elekezi kwa watumishi hao yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*

# Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali washiriki Siku ya Wanawake Duniani kwa Namna ya Kipekee





*Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakisikiliza taarifa ya Kituo cha Kulea Watoto Yatima (CHAKUWAMA) iliyosomwa na Mlezi Mkuu wa Kituo hicho Ndugu Hassan Hamis Jijini Dar es Salaam.*

Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wameshiriki shughuli mbalimbali zenye lengo la kuhamasisha usawa wa kijinsia, kuimarisha mshikamano wa kijamii na kusaidia makundi maalum katika jamii, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za kuelekea kilele cha Siku ya Kimataifa ya Wanawake Duniani iliyoadhimishwa kitaifa tarehe 8 Machi 2025, mkoani Arusha.

Katika kuadhimisha siku hiyo, wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walifanya ziara maalum katika Kituo cha Kulea Watoto Yatima (CHAKUWAMA) kilichopo Sinza, Jijini Dar es Salaam, ambapo walitoa msaada wa mahitaji mbalimbali kwa watoto wanaolelewa katika kituo hicho.

Akizungumza kwa niaba ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Hellen Lubogo, alisema kuwa msaada huo ni sehemu ya mchango wa wanawake wa ofisi hiyo katika kusaidia makundi yenye uhitaji, hasa watoto yatima. Alieleza kuwa msaada huo unalenga kuwatia moyo watoto hao na kuwahakikishia kuwa bado kuna watu katika jamii wanaowajali na kuwaunga mkono katika kutimiza ndoto zao.

Bi. Lubogo alibainisha kuwa msaada wa jiko la nishati safi ni sehemu ya jitihada za kuunga mkono kampeni ya matumizi ya nishati safi inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni kinara wa harakati hizo nchini.

Kwa upande wake, Mlezi Mkuu wa kituo hicho, Ndugu Hassan Hamis, aliishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kutambua na kugusa maisha ya watoto hao, akibainisha kuwa tangu kuanzishwa kwake mwaka 1998, kituo hicho kimeshahudumia watoto 740 na kwa sasa kinalea watoto 60 waliopo katika ngazi mbalimbali za elimu.

Mbali na msaada huo, wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali pia walishiriki mafunzo maalum yaliyolenga kuhamasisha usawa wa kijinsia, uimarishaji wa malezi ya watoto na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi. Mafunzo hayo yalifanyika Jijini Dar es Salaam na yalihusisha

mada mbalimbali ikiwemo dhima ya kauli mbiu ya Siku ya Wanawake Duniani ya mwaka 2025: "***Wanawake na Wasichana 2025: Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji.***"

Akifungua mafunzo hayo, Bi. Lubogo aliwahimiza wanawake wa ofisi hiyo kupendana, kusaidiana, na kufanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo yao ya kiuchumi na kijamii. Alisisitiza kuwa wanawake wa sasa wana uwezo wa kufanya kazi yoyote kwa ufanisi na wana nafasi kubwa ya kuchangia maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla. Alitoa wito kwa wanawake kusimama imara katika nafasi zao kwa ajili ya maendeleo ya OWMS na Taifa kwa ujumla.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Ofisi hiyo, Bi. Prisca Ulomi, alitoa mada kuhusu haki za wanawake, malezi ya watoto na umuhimu wa elimu katika kuwawezesha wanawake kiuchumi. Alisisitiza kuwa maendeleo ya wanawake ni msingi wa ustawi wa jamii na kwamba wanawake wanapaswa kutumia fursa zilizopo kwa manufaa yao na kwa vizazi vijavyo.

Kupitia shughuli hizi, wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wameonyesha mfano wa kuigwa katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa vitendo vinavyogusa maisha ya jamii, hususan makundi maalum, sambamba na kuendelea kujifunza na kujijengea uwezo kwa ajili ya ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Prisca Ulomi akizungumza na mtoto anayelelewa kwenye Kituo cha Kulelea Watoto Yatima wakati wanawake wa Ofisi hiyo walipotembelea kituo hicho kilichopo Jijini Dar es Salaam.*



*Mwenyekiti wa Wanawake TUGHE tawi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Celina Togocho akizungumza kwa niaba ya wanawake wa ofisi hiyo walipotembelea kituo cha kulea watoto yatima kilichopo Jijini Dar es Salaam.*



*Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Hellen Lubogo akitoa salamu za Ofisi hiyo kwa niaba ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali wakati wanawake wa ofisi hiyo walipotembelea kituo cha kulelea watoto yatima (CHAKUWAMA) kilichopo Jijini Dar es Salaam.*



*Mlezi Mkuu wa Kituo cha kulelea Watoto Yatima (CHAKUWAMA), ndugu Hassan Hamis akitoa taarifa kwa wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walipotembelea kituo hicho kilichopo Jijini Dar es Salaam.*



*Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa na Mlezi Mkuu na Watoto wa Kituo cha Kulelea Watoto Yatima (CHAKUWAMA) mara baada ya kutoa msaada wa vitu mbalimbali walipotembelea kituo hicho kilichopo Jijini Dar es Salaam.*



*Jiko la Nishati Safi ya Kupikia ni moja ya msaada uliotolewa na Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Kituo cha Kulea Watoto Yatima (CHAKUWAMA) kwa lengo la kuhimiza matumizi ya nishati safi.*





*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo ni miongoni mwa viongozi wa Taasisi za Serikali walioshiriki Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika Machi 08, 2025 Jijini Arusha. Mgeni Rasmi wa Maadhimisho hayo alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suhusu Hassan.*




*Baadhi ya Wanawake kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, wakipita mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungan wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika Viwanja vya Sheikh Amri Abeid Jijini Arusha.*



*Baadhi ya wananchi wakimsikiliza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati akifunga Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kitaifa katika Viwanja vya Sheikh Amri Abeid Jijini Arusha.*



*Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Hellen Lubogo akifungua mafunzo kuhusu dhima ya kauli mbiu ya Siku ya Wanawake Duniani, Malezi ya Watoto, Wanawake na Uwezeshaji Kiuchumi kwa niaba ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*





*Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Helen Lubogo (aliyeketi katikati) akiwa na baadhi ya Wanawake wa Ofisi hiyo mara baada ya kufungua mafunzo kuhusu dhima ya kauli mbiu ya Siku ya Wanawake Duniani, Malezi ya Watoto, Wanawake na Uwezeshaji Kiuchumi kwa niaba ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Prisca Ulomi akitoa mada kuhusu dhima ya kauli mbiu ya Siku ya Wanawake Duniani, Malezi ya Watoto, Wanawake na Uwezeshaji Kiuchumi yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*



*Wakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Zena Hassan akichangia mada kuhusu dhima ya kauli mbiu ya Siku ya Wanawake Duniani wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

*Baadhi ya Wanawake wa Ofisi ya Wakili ya Wakili Mkuu wa Serikali, wakimsikiliza Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi wa ofisi hiyo, Bi. Helen Lubogo (hayupo Pichani) wakati akifungua mafunzo kuhusu dhima ya kauli mbiu ya Siku ya Wanawake Duniani, Malezi ya Watoto, Wanawake na Uwezeshaji Kiuchumi kwa niaba ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*





*Afisa Tawala wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Mariam Bundala akichangia mada kuhusu Malezi ya Watoto, Wanawake na Uwezeshaji Kiuchumi wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (wa kwanza kulia) akimkabidhi zawadi ya kitabu cha upendo ndugu Yusuph Varisanga, mstaafu wa kwanza wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa hafla ya kumuaga iliyofanyika jijini Dar es Salaam.*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yamuaga Mstaafu Wake wa Kwanza

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo amewaongoza watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kumuaga ndugu Yusuph Varisanga, aliyekuwa Mtumishi wa ofisi hiyo ambaye amestaafu kwa mjibu wa sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma.

Akizungumza wakati wa hafla ya kumuga mtumishi huyo iliyofanyika kwenye viwanja vya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Mtulo alimuelezea Bw. Varisanga kama mtumishi anayepaswa kuwa mfano bora katika utumishi wa umma, kwa kuwa alikuwa mtumishi mzalendo aliyeipenda kazi yake, mchapakazi, mwadilifu na mtu mwenye nidhamu ya hali ya juu, ambaye kila mara alihakikisha anatekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa viwango vya juu.

"*Ndugu Varisanga siyo tu alikuwa mtumishi, bali pia alikuwa mshauri, mwalimu na rafiki kwa kila mtu aliye karibu nae. Alikuwa mtu wa kuaminika, mwenye moyo wa kusaidia, na asiyechagua kazi, tabia yake ya uwazi, ucheshi na ushirikiano iliwahamasisha wengi katika ofisi hii, na hakika ameacha alama isiyofutika,*" alisema Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Mtulo.

Akielezea sifa za mtumishi huyo Bi. Mtulo ameongeza kuwa Ndugu Varisanga alikuwa mtu wa kujitolea katika kila jambo linalohusu ofisi na watumishi wenzake haswa pale walipopatwa na changamoto mbalimbali, hivyo amewasihi watumishi wanaobaki kumuenzi mtumishi huyo kwa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma.

Wakizungumza kwa niaba ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mhasibu Mkuu wa Ofisi hiyo Bi. Devota Ngulugulu na Wakili wa Serikali ndugu Urso Luoga walitumia hafla hiyo kumpongeza ndugu Varisanga kwa kumaliza utumishi wa umma akiwa na afya njema na kumuelezea kuwa si tu alikuwa mtumishi pekee bali alikuwa kiongozi kwa kila mmoja wao na kueleza kuwa watamkumbuka kwa ukarimu wake



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akizungumza na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa kumuaga ndugu Yusuph Varisanga (hayupo pichani) katika hafla iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*



*Ndugu Yusuph Varisanga akitoa neno la shukurani kwa uongozi na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mara baada ya hafla ya kumuaga iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

na juhudi zake katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ambayo yamesaidia kwa sehemu kubwa ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kufikia malengo iliyojiwekea kwa wakati.

Aidha, watumishi hao walimtakia kheri na fanaka katika maisha mapya aliyoyaanza huku wakimuombea maisha marefu yenye siha njema na kumuomba kutosita kuendelea kutoa uzoefu wake pale atakapohitajika hasa katika sekta ya uhasibu na fedha ili kuendelea kuwajengea uwezo watumishi hao katika kuhakikisha ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inafikia malengo iliyojiwekea kwa wakati.

Kwa upande wake, ndugu Varisanga aliushukuru uongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na watumishi wote kwa ujumla kwa ushirikiano waliompatia wakati wote wa utumishi wake na kuwahimiza watumishi wenzake kuendelea kushirikiana, kuzingatia maadili ya utumishi wa umma ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi ili kulinda heshima ya Ofisi hiyo.

"*Nimekuwa hapa kwa muda mrefu na nimejifunza mengi kutoka kwa kila mmoja wenu. Naondoka nikiwa na furaha, kwani najua nimeacha timu ya watu wenye uwezo mkubwa na moyo wa dhati wa kulitumikia taifa. Endeleeni kushirikiana na kuheshimiana, kwani mshikamano ni msingi wa mafanikio,*" alisema ndugu Varisanga.

Watumishi hao walitumia hafla hiyo kumpa zawadi mbalimbali ndugu Varisanga kama ishara ya shukrani na kuthamini mchango wake katika utumishi wake huku watumishi hao wakifurahia kushiriki chakula cha pamoja, na kubadilishana kumbukumbu na kumbukizi za nyakati walizoshirikiana na Bw. Varisanga.

Ndugu Varisanga aliacha urithi wa uadilifu, bidii na moyo wa ushirikiano ambao hakika utaendelea kuwa mwanga kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wote watakaokuwa wakitekeleza majukumu yao ya kila siku ndani na nje ya nchi.



*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (Hayupo pichani) wakati wa hafla ya kumuaga ndugu Yusuph Varisanga iliyofanyika jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo (wa kwanza kulia) akimkabidhi zawadi ya kikombe ndugu Yusuph Varisanga wakati wa hafla ya kumuaga iliyofanyika jijini Dar es Salaam.*

*Mhasibu Mkuu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, CPA (T) Devota Ngulugulu akielezea namna walivyoshirikiana na ndugu Yusuph Varisanga wakati wa utumishi wake kwenye hafla ya kumuaga iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

*Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Mipango wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Theresia Mpangala akielezea namna walivyoshirikiana na ndugu Yusuph Varisanga wakati wa utumishi wake kwenye hafla ya kumuaga iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*





JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**
**10 Barabara ya Kivukoni**
**S. L. P 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Nukushi: www.osg.go.tz**
**Barua pepe: info@osg.go.tz**

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

| | |
|---|---|
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1902<br>41218 DODOMA<br>Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)<br>Barua pepe: dodoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 130<br>31101 MUSOMA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mara@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1280<br>63114 MTWARA<br>Maadili House<br>Barua pepe: mtwara@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 394<br>33101 MWANZA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mwanza@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 595<br>51108 IRINGA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>Barua pepe: iringa@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 106<br>35102 BUKOBA<br>Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali<br>Barua pepe: kagera@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 564<br>57101 SONGEA<br>Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 43<br>37101 SHINYANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 60<br>21101 TANGA<br>Jengo la Mkonge<br>Barua pepe: tanga@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 119<br>45112 TABORA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: tabora@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 202<br>25101 MOSHI<br>Jengo la TRA Moshi<br>Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 690<br>55103 SUMBAWANGA, Mtaa wa Ukaguzi<br>Jengo la Ukaguzi, Gorofa ya pili<br>Barua pepe: rukwa@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 66<br>23101 ARUSHA<br>Jengo la AICC, Arusha<br>Barua pepe: arusha@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 710<br>53107 MBEYA<br>Jengo la Madini<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 172<br>47101 KIGOMA, Jengo la NHC, Ghorofa ya Pili,<br>Kiwanja Na. 148 & 149, Mtaa wa Lumumba.<br>Barua pepe: kigoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>Jengo la NSSF, Ghorofa la Nne<br>MOROGORO, Barabara ya zamani DSM<br>Barua pepe: morogoro@osg.go.tz |